Hake Muhtasari No. 06k, 2016

# Je Haki ya Kupata Elimu Inatekelezwa?

## Matokeo ya Utafiti 2015

## Mapendekezo

- Idadi kubwa yya wanafunzi wa kike hawamalizi elimu yao kwa changamoto za mimba na kuolewa mapema. Serikali haina budi kuongeza mabweni hasa kwa shule za sekondari na kuweka usimamizi mzuri wa kuwasaidia wanafunzi hawa kujiepusha na vishawishi vya kupata ujauzito. Pia ni muda muafaka sasa serikali ifikirie kuwa na mpango maalumu wa kuwarudisha wanafunzi wanaopata ujauzito mara baada ya kujifungua. Katika kutekeleza hili lazima tujifunze toka kwa majirani zetu Malawi na Kenya ambao tayari wanatekeleza mpango kama huu.

- Miundombinu ya shule za msingi na sekondari si rafiki. Njia pekee ni kuwekeza kwenye ujenzi wa miundombinu na ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Serikali inabidi kuongeza bajeti ya maendeleo ya sekta ya elimu toka asilimia 15-16 hadi kufikia japo asilimia 30 ya bajeti ya sekta ya elimu.

- Uwepo wa Sheria ya Mtoto pekee hautoshi kumlinda mtoto. Ili kufanikisha hili, kunahitajika mkakati na mpango maalumu wa kutekeleza sheria hii hasa kukomesha ajira za utotoni. Elimu bure na kuweka sheria kali za kuhakikisha watoto wote wako shule na wanajifunza ipasavyo inaweza kusaidia kuondoa tatizo la ajira kwa watoto.

- Utafiti unaonesha kuwa kuna maeneo mengi ambayo yameshindwa kufanyiwa uchambuzi kwa sababu ya ukosefu wa taarifa na takwimu mbalimbali za sekta ya elimu. Hivyo katika utoaji wa takwimu za BEST serikali inabidi kuongeza takwimu nyingine kama vile za watoto wenye ulemavu, takwimu za ulinganifu kati ya mjini na kijijini, takwimu za hali ya ujinga, bajeti ya mishahara ya walimu, bajeti ya vifaa vya kujifunzia na kufundishia kwa mwaka.

RESULTS
the power to end poverty

HakiElimu inawezesha wananchi kuleta mabadiliko katika elimu na demokrasia

SLP 79401 • Dar es Salaam • Tanzania
Simu (255 22) 2151852/3 • Faksi (255 22) 2152449
info@hakielimu.org • www.hakielimu.org

hakielimu

## Utangulizi

Utafiti wa Haki ya Kupata Elimu (RTEI)[1] ni kipimo cha kimataifa kinacholenga kuonesha kiwango cha uwajibikaji wa nchi katika kufanikisha upatikanaji wa haki ya kupata elimu. Utafiti huu unatumia dodoso lenye viashiria mbalimbali vinavyopima kiwango cha utekelezaji wa Haki ya Kupata Elimu. Viashiria hivi vinazingatia mambo makuu matano ambayo ni mifumo ya sheria za utoaji elimu, idadi ya taasisi za kutoa elimu na taratibu zilizopo, ubora wa taasisi zinazotoa elimu, fursa ya kupata elimu, ubora wa elimu inayotolewa na taasisi za elimu unaokidhi mahitaji. Utafiti wa kujaza dodoso na uhakiki wa taarifa umefanywa na asasi za kiraia, taasisi za kitafiti, serikali ya nchi husika na Taasisi ya Results Education Fund. Utafiti wa mwaka 2015 umehusisha nchi tano ambazo ni Tanzania, Nigeria, Ufilipino, Chile na Zimbabwe. Matokeo yanaonesha kuwa Tanzania imepata alama nzuri kwenye eneo la fursa za kupata elimu-alama 79 kati ya 100, mifumo ya sheria na taratibu za utoaji elimu-alama 84. Ubora wa taasisi zinazotoa elimu na ubora wa elimu itolewayo bado ni changamoto kubwa. Kijarida hiki kinatoa kwa ufupi matokeo ya RTEI kwa Tanzania hasa kwenye maeneo ambayo yanahitaji maboresho zaidi.

### Jambo la 1: Uhaba wa miundombinu na vifaa ya kufundishia na kujifunzia.

Eneo hili limepata alama 43 tu kati ya 100. Tafsiri ya alama hizi ni kuwa mazingira ya kujifunzia si rafiki na kuna changamoto nyingi za miundombinu na vifaa vya kujifunzia. Kwa mfano hali ya upatikanaji wa vitabu imepata alama 27 tu kati ya 100, ikimaanisha kuwa Tanzania bado ina uhaba mkubwa wa vitabu vya kiada kwa shule za msingi ambapo wanafunzi takribani wanne wanatumia kitabu




Chati 1: Tanzania na nchi nyingine

1 Right to Education Index

kimoja badala ya kiwango cha kitaifa cha kitabu kimoja kwa kila mwanafunzi kwa kila somo. Hali ya uwepo wa madarasa pia imepata alama 13 tu kati ya 100. Uwiano wa darasa kwa wanafunzi ni 72:1. Hii inaonesha kuwa Tanzania ina changamoto kubwa sana ya uhaba wa madarasa ambapo wanafunzi 72 wanatumia darasa 1 badala ya wanafunzi 40 kutumia darasa 1. Mrundikano wa wanafunzi darasani huathiri pia ufundishaji. Kati ya nchi 5 zilizohusishwa katika utafiti wa 2015, Tanzania ndiyo imepata alama ndogo zaidi kwenye eneo hili(alama 43 kati ya 100) kama inavyooneshwa na chati namba 1.

## Jambo la 2: Elimu ya mtoto wa kike

Tanzania bado haina mazingira mazuri ya kumwezesha mtoto wa kike kupata elimu hadi ngazi za juu. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa uwiano wa watoto wa kike na wa kiume katika uandikishaji karibu uko sawa. Japo watoto wengi wa kike wanaandikishwa, idadi kubwa hushindwa kumaliza masomo yao kutokana na sababu za utoro na kupata ujauzito. Mwaka 2012 jumla ya wanafunzi wa kike 7,138 wa shule za msingi na sekondari walifukuzwa masomo kwa sababu ya ujauzito.

Pia takwimu za BEST[2] za 2014 zinaonesha kuwa asilimia 8.8 ya wanafunzi walioacha shule walitokana na kupata ujauzito. Kwa Tanzania, mwanafunzi akipata ujauzito hufukuzwa shule na wala hakuna mpango wowote wa kurudi shuleni akijifungua. Ndoa za utotoni bado ni changamoto pia ambapo hufanya watoto wengi wa kike kukatisha masomo yao ili kuolewa. Hii inasababishwa na changamoto ya sheria ya ndoa ambayo inaruhusu mtoto wa kike kuolewa mara afikishapo miaka 15, na hivyo kutoa fursa kwa mtoto wa kike kuolewa afikishapo umri wa miaka 15. Ripoti ya UNFPA ya mwaka 2012 inaonesha kuwa asilimia 36.9 ya watoto wa kike waliolewa mwaka 2010 wakiwa chini ya umri wa miaka 18. Hii pia inaonesha kuwa watoto wengi huolewa wakiwa kwenye umri wa kati ya miaka 15 hadi 18 ambao ndio umri wanapaswa kuwa shule za sekondari

2 Basic Education Statistics for Tanzania.

## Jambo la 3: Mazingira ya kujifunza na kufundishia

Katika eneo hili Tanzania imepata alama 33 kati ya 100 ikimaanisha mazingira ya watoto kujifunza si rafiki. Japo Tanzania imepitisha Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 yenye lengo la kumlinda mtoto na kukataza ajira kwa watoto chini ya miaka 15, hali imekuwa tofauti katika utekelezaji wake. Idadi kubwa ya watoto wenye umri kati ya miaka 5 hadi 14 wameajiriwa. Ripoti ya Wizara ya Kazi ya Marekani inaonesha kuwa mwaka 2013 asilimia 25.1 ya watoto wenye umri wa miaka 5-14 wa kitanzania waliajiriwa kwenye soko la ajira. Hali hii inawanyima fursa watoto kuwepo shule na kupata elimu. Changamoto nyingine ni matumizi ya viboko kwa wanafunzi ambayo huathiri mazingira ya watoto kujifunza ipasavyo. Utafiti huu unaonesha kuwa Tanzania haina sheria zinazokataza matumizi ya viboko. Sheria ya mwaka 1979 inaruhusu matumizi ya viboko na hata maelekezo ya serikali ya mwaka 2000 yanaruhusu viboko vinne na adhabu hii itolewe na mwalimu mkuu. Utafiti unaonesha kuwa bado adhabu ya viboko inatumika kiholela kwa wanafunzi tofauti na maelekezo haya ya serikali.